# Sababu kupungua sangara Ziwa Victoria yawekwa wazi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema kupungua kwa uvuvi katika Ziwa Victoria hususani samaki aina ya sangara kunatokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni uvuvi haramu.

Aliyasema hayo juzi wakati akijibu hoja mbalimbali za wabunge zilizotolewa baada ya wizara yake kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Waziri huyo alisema hali ya upatikanaji wa sangara ni mbaya ziwani huko na mkakati wao ni kudhibiti uvuvi haramu, akibainisha kuwa tangu mwaka uliopita wamekuwa wakishirikisha wadau wote wa uvuvi.

"Ni kweli tumefanya operesheni kubwa, kufanya operesheni peke yake tumegundua kwamba haitoshi, tukaona ni vizuri tushirikishe wadau wote kuanzia wavuvi wanaovua kwenye maziwa na bahari.

"Kushirikisha serikali za mitaa, halmashauri na mikoa zihusike moja kwa moja kwenye masuala haya ya kudhibiti uvuvi haramu kwa sababu serikali ni moja, huwezi kuwa na serikali inayotoka Dodoma kwenda kudhibiti uvuvi haramu Bunda au Rorya," alisema.

Waziri Ndaki alisema mkakati wao kwa sasa ni serikali nzima kuwa shirikishi na wadau nao wahusike ili wadhibiti hilo.

Alisema wanafahamu samaki ni rasilimali inayomsaidia kila Mtanzania na wakisaidia leo halafu kesho wasifanye hivyo, ni bahati mbaya.

Alisema wanaendelea kutoa elimu ya uvuvi endelevu kwa wavuvi na kufanya maboresho ya kanuni ili wadhibiti sawasawa suala hilo.

Kuhusu viwanda vilivyofungwa, alisema siyo lazima vifungwe kwa sababu sangara hawapo, bali vipo vilivyofungwa kwa matatizo ya uongozi na uendeshaji. "Siyo sawa kusema viwanda vimefungwa kwa sababu sangara walikuwa kidogo," Waziri Ndaki alitoa angalizo.

Awali, akichangia bajeti hiyo, Mbunge wa Viti Maalum, Mariam Ditopile, alisema hali ya upatikanaji wa samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria ni mbaya na hafahamu kama kwenye vipaumbele vya wizara hiyo wameliona hilo.

"Kwanini ninasema hali mbaya, sangara ni bidhaa katika soko la samaki la duniani, Ulaya ndiyo soko kubwa ambalo zaidi ya asilimia 70 ya mazao ya samaki yanayotoka Afrika yanakwenda huko.

"Mwaka 2014/15 Tanzania tulikuwa tunatoa tani zaidi ya 45,000 za minofu ya sangara na mazao yake lakini mwaka 2021 tumetoa tani 14,000 tu , lakini viwanda vyetu vimekuwapo mwaka 2014/15 tulikuwa tunaajiri zaidi vijana 12,000 kwenye sekta hii. Akiendelea kujibu hoja mbalimbali, Waziri Ndaki pia alizungumzia leseni za uvuvi wa bahari kuu, akisema kuwa kwa mujibu wa kanuni ya usimamizi na uendelezaji wa uvuvi wa bahari kuu ya mwaka 2021, bei za leseni za uvuvi eneo hilo kwa meli za Kitanzania zilipunguzwa kati ya asilimia 70 hadi asilimia 86 kulinganishwa na za leseni kwa meli za kigeni.

Waziri Ndaki alisema wana mpango wa kutoa boti 320 ambazo zitakuwa na upekee, ndani yake zikikuwa na vifaa mbalimbali ikiwamo GPS, vifaa vya ubaridi, 'fishing finder' zitakuwa na uwezo wa kubeba tani 1.5.



Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti

# Dunia yaungana kudhibiti ufugaji kuku katika vizimba

## Yasisitiza ufugaji huria kwa ustawi wa kuku

Hadi kufikia Aprili 2022, asilimia 88 ya kampuni zilizotoa ahadi ya matumizi ya mayai ambayo hutagwa na kwa kutumia ufugaji huria wa kuku, zimetimizwa matakwa hayo.

NA MWANDISHI WETU

KATIKA kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022, kumekuwepo makubaliano ya kisera ya kukomesha ukatili dhidi ya kuku na kitiwa saini zaidi ya mashirika 500 duniani ambapo Bara la Afrika yapo mashirika 15 ambayo yamekubali ukomeshaji wa ukatili dhidi ya kuku.

Aidha, zaidi ya mashirika 2,300 ya chakula dunia yamepitisha sera za ustawi wa kuku ambazo huondoa vizimba vinavyotumika kufuga kuku wanaotaga mayai ambapo kampuni 982 zimekamilisha kwa ufanisi ufugaji kuku wa mayai matumizi ya vizimba vya betri.

Hadi kufikia Aprili 2022, asilimia 88 ya kampuni zilizotoa ahadi ya matumizi ya mayai ambayo hutagwa na kwa kutumia ufugaji huria wa kuku, zimetimizwa matakwa hayo.

Ili kuhakikisha mkakati huo unafikiwa, Mei 16, 2022 Shirika linalotetea haki za wanyama Open Wing Alliance (OWA) ilizindua ripoti ya ufugaji huru ya mwaka 2022.

Ripoti hiyo ya pili iligusia uzalishaji mayai yatokanayo na ufugaji huria wa kuku ambapo ripoti hiyo inatoa fursa kwa kila kundi na umma kuelewa kwamba kampuni nyingi zinatimiza ahadi zao za ustawi wa wanyama, lakini kuna baadhi ya kampuni ambazo zinarudi nyuma linapokuja suala la maendeleo, uwazi katika haki za wanyama.

Muungano wa The Open Wing Alliance duniani, umekuwa ukifanya kazi bila kuchoka kuhakikisha kunakomeshwa matumizi ya kikatili ya kuwafungia kuku wanaotaga mayai kisha kuingizwa katika mfumo wa chakula hasa viwandani.

Muungano huo unahusisha zaidi ya mashirika 80 kutoka nchi 63 ambayo yamekuwa yakifanya kazi kwa zaidi ya muongo mmoja ili kupata ahadi ya kukomesha ukatili dhidi ya kuku kutoka kwa kampuni kubwa zaidi za chakula duniani.

Tanzania nayo haiko nyuma katika mapambano dhidi ya ukatili wa wanyama, kwani OWA imekuwa ikishirikiana na mashirika mbalimbali ya ustawi wa wanyama.

Miongoni mwa mashirika hayo ni shirika la Education for African Animals Welfare (EAAW) katika kutekeleza shughuli zake hususan utoaji wa elimu na kampeni zinazolenga kukomesha ukatili dhidi ya wanyama hasa kuku waliofungiwa kwenye vizimba.

Akizungumzia mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya kuku, Mkurugenzi wa OWA, Alexandria Beck, anasema kuendelea kupata ahadi nyingi katika kutekeleza sera ya ustawi wa wanyama, ni kiashirio muhimu cha maendeleo kwa wanyama wanaofugwa kwa ajili ya chakula.

"Ingawa tunajua kwamba ahadi pekee hazitasababisha kuboreshwa kwa hali za wanyama. Ili kuwaokoa kuku kutokana na maisha ya ukatili ya kufungiwa kwenye vizimba vya chuma, tunahitaji kuona kampuni zinatengeneza na kutoa taarifa kuhusu maendeleo kuelekea malengo yao ya ufugaji huria," anaeleza.

Beck anasema takwimu zinaonyesha kwamba siku zijazo hakutakuwa na ufugaji wa vizimba na zaidi ya asilimia 11 ya kuku duniani, hawafugwi katika vizimba.

Yapo baadhi ya mashirika ambayo yana sera ya kuondoa matumizi ya vizimba katika kufikia asilimia 100 ya mayai yatokanayo na kuku wasiofugwa kwenye vizimba, bado hawajaweka wazi hadharani maendeleo yao ya hatua iliyofikiwa katika maeneo yao.

Miongoni mwa kampuni hizo ni Hilton Hotels, Radisson Hotels Group na Unilever. Hata hivyo, barani Afrika kuna mashirika yaliyofikia na kutimiza ahadi ya uondoaji vizimba katika ufugaji wa kuku, ambayo ni Danone, Marriott, Starbucks na Kraft Heinz ambayo yanaripoti kwa uwazi hatua zilizofikiwa.

Mapema mwaka huu, kampuni ya kimataifa ya Majid Al Futtaim ambao ni wauzaji wakubwa wa mazao ya kuku kupitia maduka ya Carrefour nchini Kenya, Kameruni, Uganda na Misri walitoa ahadi ya kutekeleza sera ya kimataifa yakutofungamana na wauzaji mayai ya kuku wanaofugwa katika vizimba.

Majid Al Futtaim ilionyesga namna ambavyo watumiaji wa mayai wanavyojali ustawi wa wanyama. Hata hivyo bado kuna changamoto kwa ustawi wa kuku katika ukanda wa Afrika, kwani zipo kampuni zimekuwa zikisuasua kukubaliana na sera ya uondoaji vizimba kwa kuku wa mayai wanaofugwa.

Pia, wauzaji wa mayai kwa reja reja kama vile Pick n Pay, Shoprite na Massmart, wanahitaji kujitolea zaidi kwa kusisitiza ufugaji kuku bila vizimba ili kudhihirisha kwa umma kwamba wanajali ustawi wa wanyama hususan kuku.



Nukuu



"Hatuingii kwenye uandishi wa hab
kutafuta ukweli na kuhakikisha vio

Helen Thomas, mwanahabari wa Mareka

MWANANCHI UK 10

# Sekta ya mifugo, uvuvi iamke sasa

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetangaza vipaumbele vitano inavyotarajia kuvitekeleza katika bajeti yake ya mwaka wa fedha wa 2022/23.

Akizungumza na *Mwananchi* baada ya kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake bungeni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema kuwa vipaumbele vya makadirio ya bajeti mpya ni vitano ambavyo ni uhimilishaji, malisho na maji, tiba na kinga ya magonjwa na ujenzi wa bandari ya uvuvi inayokwenda kujengwa mkoani Lindi.

Alisema watajenga uboreshaji wa malisho na maji sambamba na kuanzisha madarasa 100 ambayo yatakuwa yanamilikiwa na mfugaji mmoja. Alisema katika kipaumbele cha tiba na kinga kwa magonjwa, watajenga zaidi ya majosho 300 nchi nzima.

Kuhusu uvuvi ambao pia unasimamiwa na wizara hiyo, alisema mwaka huu wataanza ujenzi wa bandari ya uvuvi eneo la Kilwa Masoko mkoani Lindi.

"Kwa kufanya hivyo, meli kubwa za uvuvi zimeanza kuja na tumezipa leseni (ya kuvua), ziweze kutia nanga," alifafanua Waziri Ndaki.

Ukitazama kwa undani, vipaumbele hivi vinaleta matumaini ya kuwapo kwa dhamira ya kuiletea mabadiliko sekta ya mifugo nchini, ambayo kwa muda mrefu haijawa na tija kama inavyotarajiwa na wadau wake na hata jamii kwa jumla.

Licha ya nchi yetu kitakwimu kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa kuwa na mifugo mingi barani Afrika, si mifugo hiyo wala bidhaa zitokanazo na mifugo hiyo, vilivyo na mchango wa maana katika uchumi wa Taifa.

Pamoja na faida chekwa zitokanazo na sekta ya mifugo kama vile uzalishaji wa nyama, maziwa, kwato, ngozi na mbolea, ufugaji nchini hauchangii vya kutosha kwenye uchumi na ajira, hali inayotokana na kutokuwapo kwa mipango mizuri na thabiti ya kuwaendeleza wadau wake, hasa wafugaji wadogo ambao ndio wengi.

Kwa muda mrefu ufugaji umekuwa wa mazoea, wa holela na ule wa kiasili wa kuhamahama, hivyo kusababisha mifugo kutokuwa na sifa hata pale soko la maana linapopatikana. Na ni kama vile Serikali kupitia mamlaka zake husika, zimeshindwa kuwakalisha kitako wafugaji hawa wakaondokana na ufugaji wa mazoea wakumbatie ufugaji wa kisasa ambapo mfugaji anakuwa na mifugo michache anayoimudu na hivyo kuihudumia ipasavyo.

Tunapopigia chapuo sekta hii kusimamiwa vilivyo kupitia mikakati na mipango thabiti, ieleweke kuwa sekta ya mifugo haichangii tu kwenye uchumi kwa kukuza pato la Taifa au kuongeza ajira, lakini ufugaji ni chanzo cha uhakika cha chakula, lishe ya uhakika na malighafi za viwanda.

Ni kwa sababu hiyo, tunazikumbusha mamlaka husika, ikiwamo Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuimarisha sekta hii muhimu na nyeti. Tuondokane na ufugaji wa mazoea, na sasa tugeukie kwenye ufugaji wa kisasa kwa Serikali kutenga maeneo ya malisho, vyanzo vya maji, huduma za utafiti na mafunzo kwa wadau wote wa sekta hiyo.

Vipaumbele vitano alivyovitaja Waziri Ndaki, vitufumbue macho na kuona haja ya kuwekeza vilivyo kwenye sekta hii ambayo kama Taifa, tukijipanga vilivyo inaweza kuwa chanzo kizuri cha mapato kwa kuwa bidhaa zitokanazo na mifugo sio tu zinatumika sana kila kona ya dunia, lakini pia zina faida nyingi za kiuchumi.